



# Siwa la Kiswahili

**Kijarida cha Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Toleo la 1**



## Dibaji

Nawakaribisha kujisomea toleo la sasa la *Siwa la Kiswahili*. *Siwa la Kiswahili* hutolewa na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Idara ya lugha ya Kiswahili licha ya uchanga wake ni kisima cha utafiti katika fani tofauti za fasihi na lugha yake.

Licha ya utafiti wa vitengo tofauti, Idara ya Kiswahili ni dafina ya kazi mbalimbali za waandishi wenye uzoefu mkubwa. Waandishi huandika hadithi fupi, riwaya, mashairi na hata insha za kifasihi.

Kijarida chetu cha *Siwa la Kiswahili* kimekusanya picha za baadhi ya hawa waandishi watajika pamoja na wanafunzi wao. Ningependa kukuomba wewe msomaji ujumuike nasi katika uhondo huu unaofichuliwa na kijarida cha mtandao kwa kuijua zaidi na hata kuweza kuitolea maoni Idara ya Kiswahili na juhudi zake.



**Prof. John H. Habwe**  
Mwenyekiti, Idara ya Kiswahili

## Yaliyomo

Dibaji.....	1
Ngazi ya mhariri.....	2
Kongole.....	3
Wahadhiri wa idara.....	4
Uchapishaji.....	8
Wanafunzi wa uzamili...12	
Mapokezini.....	14
Masomo.....	16
Ushirikiano.....	17
Habari za visiwani.....	18

## Ngazi ya Mhariri

Wapendwa wasomaji,  
Hili ni toleo la mwanzo la kijarida cha Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Wafahamu wahenga walisema kuwa kwanza kwa saburi, kwisha kwa sururi? Tunaamini kuwa siku njema ndiyo hii na kwamba daraja livuke ulifikia...tumelifikia na sasa tumevuka kwa kukizindua kijarida hiki kwenye mtandao.



Kama alivyodokeza mwenyekiti wa Idara Prof. Habwe katika dibaji ya toleo hili, Idara hii ya Kiswahili imechangia pakubwa katika fasihi ya Kiswahili na maswala ya lugha kwa jumla. Baadhi ya kazi zilizochapishwa za baadhi ya wahadhiri zimetajwa. Vile vile, ni nani anayehusika na ufundishaji wa Kiswahili Idarani? Tumetaja baadhi ya kozi zinazofundishwa hapa na wahadhiri wahusika katika viwango vya uzamili na shahada ya kwanza. Pia wanafunzi wetu wa shahada ya uzamili katika mwaka wa masomo wa 2012/2013 wametajwa.

Kijarida hiki kitakuwa kikikupa habari za utamaduni kutoka visiwani. Kwenye toleo hili, zipo habari kuhusu sherehe za maulidi. Tungependa kupata maoni yako kuhusu kijarida hiki kupitia anwani ya barua meme ya mhariri([tom.mboya@uonbi.ac.ke](mailto:tom.mboya@uonbi.ac.ke))  
Karibuni!

***Dkt. Tom Olali, Mhariri***



## Kongole

Walezi wa Kiswahili, Isimu na Fasihi yake, ninaomba kutoa shukrani za kipekee kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa Kutuzalia mtoto muhimu - Idara ya Kiswahili. Tumetazamia uwepo wa idara hii kwa siku nyingi.

Ninafurahi sasa kwamba ninaporudi tena kusomea shahada ya pili, ombi la kuzaliwa kwa idara ya Kiswahili tayari lishajibiwa. Kongole na ninawahongeza walezi wote wa Kiswahili waliopigania kuzaliwa kwa mtoto huyu, kwa kazi faridi na kubwa ya kujitolea.

***Henry Indindi, mpenzi na mlezi wa Kiswahili***

Ni furaha kubwa kwa kuzinduliwa kwa Idara ya Kiswahili. Sisi kama wanatusima tunawapa kongole. Mwenye-Ezi-Mungu awape neema na kukuza Idara hii ambayo sasa ni mojawapo ya turathi za taifa letu la Kenya.

***Prof. Sheikh Ahmed Nabhany, RISSEA, Mombasa.***

Kwa furaha na vicheko, twawapa hongera kwa kuanzisha Idara ya Kiswahili.

***Dkt. Issa Mwamzandi, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret***



## Wahadhiri wa Idara ya Kiswahili

Kutana na wahadhiri wa Idara ya Kiswahili. Kila mhadhiri amebobea eneo lake. Njoo Idarani ukutane nao ili umakinike!



**Dkt. Rayya Timammy**



**Dkt. Tom**



**Bi. Hannah C. Mwaliwa**



**Dkt. M**



**n Olali**



**Prof. John Habwe**



**Dkt. Iribe Mwangi**



**ichira Nyachae**



**Dkt. Hezron Mogambi**



## Wahadhiri wa Idara ya Kiswahili

Hawa ni wahadhiri wako wa Kiswahili wenye ujuzi wa juu katika lugha ya Kiswahili. Ni kundi ambalo liko mbele katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili!



**Dkt. Kineene wa Mutiso**



**Bi. Margaret Njuguna**



**Dkt. Musyoka Mwangangi**



**Dkt. Zaja Omboga**



**Dkt. Prisca Jerono**



**Mw. Basilio Mungania**



## Wahadhiri wa Idara ya Kiswahili



**Dkt. Swaleh Amiri**



**Dkt. Ayub Mukhwana**



**Dkt. Evans Mbutia**

Umezisoma ri-  
waya za Profesa  
Wamitila?  
Nikupe kazi?  
Nenda kaisome  
*Harufu ya mapera!!*



**Prof. Kyallo Wadi Wamitila**




**Dkt. Mwenda Mbatiah**




**Prof. Mohammed Hassan Abdulaziz**

Baba wa  
Idara ni  
Prof. Ab-  
dulaziz...t  
unakuvul-  
-ia kofia.




## Uchapishaji

## Riwaya



Wahadhiri katika idara hii wanajizatiti kuchangia pakubwa kukuza fasihi ya Kiswahili kupitia riwaya. Riwaya hizi zimeshinda tuzo mbalimbali.





## Uchapishaji

### Jarida

Wahadhiri hapa ni wanachama wa Chama cha Kiswahili cha Taifa (Chakita). Wameandika makala mbalimbali zilizokusanywa kwenye *Ukuzaji wa Kiswahili*

**UKUZAJI WA KISWAHILI**  
Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali

Inakiwa kwamba lugha ya Kiswahili hazungumzwa na zaidi ya watu milioni 100 ulimwenguni kote. Kati ya wazungumzaji hawa, ni taliban watu milioni mbili tu ambao wanazungumza Kiswahili kama lugha ya mama. Vilevile, mbali na Kiarabu, Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika yenye wazungumzaji wengi zaidi ulimwenguni. Hali hi inamaanisha kwamba Kiswahili kinaendelea kutanda na kuenea katika pembe zote za ulimwengu na kutika katika jaribu za mbali kutoka katika chimbuko lake. Hivi sasa, Kiswahili kinafundishwa na kutafitiwa katika vyuo vikuu mbalimbali sio tu hapa barani Afrika, bali pia Marekeni, Ulaya, Asia na kwa hakika ulimwenguni kote. Istoshe, Kiswahili ni lugha ya mawasiliano katika Afrika Mashariki na Kati pamoja na kwamba ni lugha taifa na/au lugha rasmi katika mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kutoa, kusambaa na kuimarika kwa Kiswahili kumetokana na sababu mbalimbali kama vile biashara, ushirikiano wa kimataifa, utalii na usafiri na utandawazi miongoni mwa sababu zingine. Pamoja na hayo, kuna asasi nyingi ambazo huhusika katika ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili katika mataifa na maeneo tofautitofauti. Asasi hizo ni pamoja na taasisi za elimu, bunge na vyombo vya utungaji sera, vyombo vya habari na mawasiliano, idara za Kiswahili katika vyuo vikuu, dini, sekta ya uchapishaji, na kadhalika. Katika *Ukuzaji wa Kiswahili: Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali*, wataalamu watajika wa Kiswahili wanachanganua na kutathmini mchango wa asasi hizo katika ukuzaji wa Kiswahili. Wataalamu hao wametoka mataifa tofautitofauti kama vile Unguja, Marekeni, Urusi, Japani, Tanzania na Kenya. Aidha, wataalamu hao wanasagaza changamoto zilizo na kutoa mapendekezo ambayo yakitingatwa, yatapeleka Kiswahili kuimarika hata zaidi ili kiweze kuwa chombo muhi cha mawasiliano, ustawi na maendeleo katika nyakati hizi za utandawazi na teknolojia ya habari na mawasiliano. Hiki ni kitabu muhimu kwa wapenzi na wasomi wa Kiswahili.

ISBN 9966-01-211-9

**FOCUS**  
TAFIRI WA KISWAHILI

Nyachae Michira • P. I. Iribemwangi • Mwenda Mbatiah  
(Wahairi)

## Tafsiri

WILLIAM SHAKESPEARE

**Othello**

Iago ameapa kulipiza kisasi kwa kuivuruga ndoa ya Othello na Desdemona. Njia pekee ya kufanikisha lengo lake ni kumghilibu Othello kwa mkewe ni mwasherati.

Je, Iago alifaulu katika azma yake? Je, Othello alizikabali bila za Iago? Endapo Othello alishawishika, alimchukulia hatua gani Desdemona?

Haya ni kati ya maswali anayoyajibu William Shakespeare katika tamthiliya hii ya tanzia inayoburudisha, kufaniza na kukaidi mpito wa wakati. Tafsiri hii imeandikwa kwa ufundi mkubwa hivi kwamba ule mvuto na mnato wa kazi asilia umedumishwa.

Dkt. Ayub Mukhwane ni mhadhiri katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi. Yeye, vilevile, amejizolea sifa katika fani ya tafsiri humu nchini na nje ya nchi.

Dkt. P. I. Iribemwangi ni mhadhiri mwandamizi katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi. Yeye ni mwandishi mwenye tajiriba pana katika fasihi ya Kiswahili, pamoja na kuwa ni mtaalamu katika tafsiri.


OXFORD UNIVERSITY PRESS

www.oxford.co.ke

ISBN 978 019 573810 0

**OXFORD**


Idara hii pia inajivunia kuwa na wataalamu ambao wamechangia kuendeleza fasihi ya Kiswahili kupitia kazi za tafsiri. Tamthilia ya kusifika ya *Othello* ni mojawapo ya tafsiri za Kiswahili zilizofanywa na wahadhiri hapa.




## Uchapishaji

### Novela

Mbali na riwaya, wadhiri wanaandika novela, vitabu vya marejeo na hadithi fupi.




### Hadithi Fupi



### Marejeo



Baadhi ya vitabu vya marejeo vinalenga sherehe za milad-un-nabi(maulidi) zina-zofanyika kisiwani Amu.



## Uchapishaji



Tasnifu za umahiri(uzamili) na uzamifu zinatiliwa mkazo idarani. Tasnifu hizi zinaangazia fasihi, isimu ya lugha ya Kiswahili, isimu jamii na sanaa za maonyesho. Ni sharti kila mwanafunzi anayepata shahada hizi kuandika tasnifu kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada hizo Tasnifu lazima iwe ni kazi ya mwanafunzi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.



## Wanafunzi wa shahada ya uzamili mwaka wa masomo 2012/2013



**Mary Nyambura**



**Emaitta Murugu**



**Anne Njoroge**

Wanafunzi wetu wa shahada ya pili hupewa mafunzo ya isimu, fasihi na njia za utafiti. Hapa idarani huwa tunawahimiza washauriane na wahadhiri wao ili wasikanyage chechele!



**Ann Raitania**

Kwa habari zaidi kuhusu masharti ya kujiunga na idara yetu kama mwanafunzi wa shahada ya pili, wasiliana na ofisi za masomo ya juu kwa nambari 318262 (ulizia 8559) ama wasiliana na Peris kwa nambari 318262 (ulizia 28063).



**Millicent Sabula**



Tabasamu zao ni dhihirisho kuwa wanafurahia masomo yao!



**Rose Kaumeuru**



**James Mburu**



**Simon Kilanga**



**Mhadhara wa somo la Nathari ya Kiswahili**



## Mapokezini



**Bi. Josephine Wanjiku na Bw. Simon Eshirere**



**Bi. Peris Kemei**

K Utahudumiwa mara moja na wenzetu wa mapokezini. Ikiwa ungependa kukutana na mwenyekiti wa Idara Profesa John Habwe, basi utaelekezwa ofisi nambari 311. Kama hayupo, utashauriwa kukutana na mhadhiri yeyote yule idarani kukuhudumia. Jambo la msingi ni kuwa hutarudi bila kupata huduma ya namna moja ama nyingine. Wageni wote wanakaribishwa.



**Anwani ya Mhariri**

**Dkt. Tom Olali**

**Simu: 318262 (uliza 28047)**

**Barua pepe: [tom.mboya@uonbi.ac.ke](mailto:tom.mboya@uonbi.ac.ke)**

## Baadhi ya masomo yanayotolewa idarani (Shahada ya kwanza)



- CLK 101: Listening Skills and Oral Communication in Kiswahili( Dkt. Jerono)
- CLK 102: Introduction to Translation and Interpretation (Dkt. Mogambi)
- CLK 103: Introduction to Kiswahili Prose(Dkt.Mbatiah)
- CLK 104: Introduction to Kiswahili Linguistics(Ms. Mwaliwa)
- CLK 203: Kiswahili and the Media(Mr. Mungania)
- CLK 302: Literary Theories and Criticism of Kiswahili Literature
- CLK 303: Performing Arts in Kiswahili(Dkt. Olali)
- CLK 402: Research Methods and Academic Writing (Dkt. Zaja Omboga)
- CLK 404: Kiswahili Oral Literature and Culture(Dkt.Olali)

## Baadhi ya masomo yanayotolewa idarani (Shahada ya uzamili)

- CLS 502: Swahili Drama (Prof.Wamitila)
- CLS 504: Epic and Long Poem (Dkt. Kineene wa Mutiso)
- CLS 506: Advanced Morphology (Mr. Mungania)
- CLS 601: Swahili Syntax (Prof. Abdulaziz)
- CLS 603: Swahili Prose (Dkt.Olali)
- CLS 605: Sociolinguistics (Dr.Mukhwana)
- CLS 602: Semantics and Pragmatics (Prof.Habwe)



## Ushirikiano



**Wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Tianjin Normal nchini Uchina wakiwa na mwalimu wao Dkt. Tom Olali.**

Idara yetu inashiriki kutoa mafunzo ya Kiswahili kule Chuo Kikuu cha Tianjin Normal nchini Uchina. Kila mwaka, mhadhiri mmoja kutoka idara yetu anamaliza kipindi cha mwaka mmoja akifundisha Kiswahili chuoni humo. Kwa upande wake, Chuo Kikuu cha Tianjin huwatuma walimu wake kufundisha lugha ya kichina kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Juhudi zinaendelea kuviingiza vyuo vikuu vingine kote ulimwenguni kuwa na ushirikiano wa namna hii na idara yetu.

## Habari za visiwani Na Tom Olali



Makala ya *habari kutoka visiwani* kwenye toleo hili linamulika sherehe za maulidi. Neno maulidi linatokana na neno la Kiarabu *Milan-un-nabi* ambalo linaashiria kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammed (S.A.W). Idara yetu inajihusisha ipasavyo na utafiti wa sherehe hizi. Katika karne ya 20, mji wa Lamu umekuwa mahali pa sherehe hizi inayowavutia wageni kutoka pande zote za Uswahilini na nchi za mbalimbali zikiwemo Uingereza na Marekani. Sheikh Habib Swaleh Jamal Leil al Habshi alifika Lamu kutoka Hadramaut (Yemeni) katika miaka ya 1880 akafundisha kwenye madrasa. Yeye ndiye aliyejenga msikiti wa Riyadhha ama *Ribat ar-Riyada* mnamo mwaka 1900. Chini ya uongozi wake, sherehe ya maulidi ikasheherekewa na wanafunzi wake wengi walioimba kasida za kumsifu na kumtukuza mtume Muhammed(S.A.W). Sherehe hizi zimeendelea kuwavutia washiriki na watazamaji wengi hata baada ya kifo chake mwaka 1935.



Mwandishi na Maalim Al-Dini kiongozi wa mabingwa wa Pate aki-kangaya beti za *Kasidatul al-Hamziyyah* wakati wa sherehe za maulidi, Lamu.